

# Zana ya kuchunguza shule na makao ya watoto dhidi ya COVID-19

Toleo la 2: Oktoba 1, 2020

Lazima watoto wachunguzwe COVID-19 kila siku kabla ya kwenda shulen au kwenye makao ya watoto. Wazazi wanaweza kujaza hati hii kwa niaba ya mtoto.

## Maswali ya Uchunguzi (weka "X" kwenye safu inayofaa)

1. Je, mtoto wako ana mojawapo wa dalili **mpya au zinazohofisha** kati ya zifuatazo? Dalili hazipaswi kuwa hatari au zinazohusiana na vyanzo au hali zingine zinazojulikana.

Homa na/au baridi (halijoto ya 37.8°C/100.0°F au zaidi)	<input type="checkbox"/> Ndiyo	<input type="checkbox"/> Hapana
Kikohozi (zaidi ya kawaida ikiwa ni kikohozi hatari) ikiwa ni pamoja na kifaduro (kikohozi kikuu, kutoa sauti ya kupuliza wakati unapumua)  Haihusiani na chanzo au hali zingine zinazojulikana (k.m., pumu, matatizo ya upumuaji)	<input type="checkbox"/> Ndiyo	<input type="checkbox"/> Hapana
Upungufu wa pumzi (kuhisi kutopumua hewa ya kutosha (dyspnea), kuishiwa na pumzi, kushindwa kupumua kwa undani, kokorota vibaya kuliko kawaida ikiwa kuna upungufu hatari wa pumzi)  Haihusiani na chanzo au hali zingine zinazojulikana (k.m., pumu)	<input type="checkbox"/> Ndiyo	<input type="checkbox"/> Hapana
Kupungua au kupoteza hisia za harufu au ladha (matatizo mapya ya kunusa au ladha)  Haihusiani na chanzo au hali zingine zinazojulikana (k.m., uvimbe wa ndani ya pua, mizio, matatizo ya neva)	<input type="checkbox"/> Ndiyo	<input type="checkbox"/> Hapana

2. Je, mtoto wako ana mojawapo ya dalili **mpya au zinazohofisha** kati ya zifuatazo? Dalili hazipaswi kuwa hatari au zinazohusiana na vyanzo au hali zingine zinazojulikana.

Kuashwa koo (uchungu au matatizo ya kumeza)  Haihusiani na chanzo au hali zingine zinazojulikana (k.m., kikohozi kinachoziba koo mara kwa mara, kurudi kwa asidi kwenye umio)	<input type="checkbox"/> Ndiyo	<input type="checkbox"/> Hapana
Pua liliolfungamana na/au linalotoa kamasi (kufungamana kwenye pua na/au utoaji wa kamasi nyepesi wakati wote)  Haihusiani na chanzo au hali zingine zinazojulikana (k.m., mizio ya msimu, kurudi ndani kutoka kwa baridi, uvimbe hatari puanisi obadilika kutoka kawaida, kuashwa kwa mkondo wa hewa.)	<input type="checkbox"/> Ndiyo	<input type="checkbox"/> Hapana
Maumivu ya kichwa ambayo ni mapya na yasiyopona, yasiyo ya kawaida, yasiyolelezeka au ya kudumu  Haihusiani na chanzo au hali zingine zinazojulikana (k.m., maumivu ya kiasi ya kichwa, kipandauso hatari)	<input type="checkbox"/> Ndiyo	<input type="checkbox"/> Hapana
Kichefuchefu, kutapika na/au kuhara  Haihusiani na chanzo au hali zingine zinazojulikana (k.m., kutapika kwa muda mfupi kwa sababu ya wasiwasi kwa watoto, matatizo hatari ya masikio, ugonjwa wa kuashwa kwa tumbo, ugonjwa wa uvimbe wa tumbo, athari ya dawa)	<input type="checkbox"/> Ndiyo	<input type="checkbox"/> Hapana
Uchovu, kukosa nguvu, maumivu ya misuli au unyonge (hisia ya jumla ya kutokuwa sawa, ukosefu wa nguvu, uchovu uliokithiri, matatizo ya kula kwa watoto wachanga) amba si kawaida au hauelezeki.  Haihusiani na chanzo au hali zingine zinazojulikana (k.m., mfadhaiko, kukosa usingizi, ugonjwa wa tezi, anemia)	<input type="checkbox"/> Ndiyo	<input type="checkbox"/> Hapana

3. Je, mtoto wako amesafiri nje ya Kanada katika siku 14 zilizopita?  
 Ndiyo  Hapana
4. Je, mtoto wako ametambuliwa kutangamana kwa karibu na mtu aliyethibitishwa kuwa na COVID-19 na kitengo cha afya cha umma cha eneo lako (au kutoka kwa programu ya COVID Alert ikiwa ana simu yake)?  
 Ndiyo  Hapana
5. Je, mtoto wako ameshauriwa kujitenga na daktari ikiwa ni pamoja na afisa wa afya ya umma?  
 Ndiyo  Hapana

## Matokeo ya Maswali ya Uchunguzi

! Iwapo umejibu "NDIYO" kwa dalili zozote zilizojumuishwa chini ya swali la 1:

- Mtoto wako anapaswa kukaa nyumbani ili kujitenga mara moja.
- Wasiliana na mtoe huduma wa afya ya mtoto wako kwa ushauri au uchunguzi zaidi, ikiwa ni pamoja na iwapo mtoto wako anahitaji kupimwa COVID-19 au matibabu mengine.

! Iwapo umejibu "NDIYO" kwa moja tu ya dalili zilizojumuishwa chini ya swali la 2:

- Mtoto wako anapaswa kukaa nyumbani kwa saa 24 kutoka wakati dalili ilianza.
- Iwapo atapata nafuu, mtoto wako anaweza kurudi shuleni/makazi ya watoto wakati atakapojisikia vizuri kufanya hivyo. Akipatikana kuwa na COVID-19 hatatakiwa kurudi shuleni.
- Iwapo dalili itaendelea au kuhofisha, wasiliana na mtoe huduma wa afya ya mtoto wako kwa ushauri au uchunguzi zaidi, ikiwa ni pamoja na iwapo mtoto wako anahitaji kupimwa COVID-19 au matibabu mengine.

! Iwapo umejibu "NDIYO" kwa dalili mbili au zaidi zilizojumuishwa chini ya swali la 2:

- Mtoto wako anapaswa kukaa nyumbani ili kujitenga mara moja.
- Wasiliana na mtoe huduma wa afya ya mtoto wako kwa ushauri au uchunguzi zaidi, ikiwa ni pamoja na iwapo mtoto wako anahitaji kupimwa COVID-19 au matibabu mengine.

! Iwapo umejibu "NDIYO" kwa swali la 3, 4 au 5:

- Mtoto wako anapaswa kukaa nyumbani ili kujitenga mara moja na kufuata ushauri wa afya ya umma.
- Iwapo mtoto wako anapata dalili zaidi, unapaswa kuwasiliana na kitengo cha afya cha umma cha eneo lako au mtoe huduma wa afya ya mtoto wako kwa ushauri zaidi.

! Iwapo umejibu "HAPANA" kwa maswali yote, mtoto wako anaweza kwenda shuleni.

## Afya ya Umma ya Ontario - Kufuatilia Walio tangamana na Mgonjwa

Kujibu maswali haya ni kwa hiari. Maelezo haya yatatumiwa tu na maafisa wa Afya ya Umma ili kufuatilia walio tangamana na mgonjwa. Maelezo yote yatafutwa baada ya siku 28.

Tarehe: \_\_\_\_\_

Jina: \_\_\_\_\_

Nambari ya simu au email: \_\_\_\_\_